**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE**

SHULE YA SEKONDARI MAKETE WASICHANA,
S.L.P. 36,
MAKETE
Tarehe ........................

**Kumb. Na.MGSS/JI/VOL 1/2026/11**
**NDUGU MZAZI/MLEZI WA .................**
**..........................................................**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO MWAKA .....................**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shule ya sekondari Makete wasichana kulingana na chaguo lako ___________ Shule itafunguliwa tarehe ________________ shule yetu ina tahasusi (Combinations 4**)** **HKL, HGK, HGFa na HGLi**. Shule ipo wilaya ya Makete Mkoa wa Njombe, Km43 kutoka Makete mjini na Km 84 kutoka Njombe stendi kuu ya mabasi. Usafiri wa mabasi upo kila siku kuanzia Njombe stendi kuu ya mabasi hadi Ikonda, Kuanzia asubuhi kuna kampuni za **Japanese, Penguin, Usalule, Mungu ni mwema, Shalom Halisi, Super Feo, Masihi, Ubaruku one, Super Rojas na Sikinde,** zinazo fika ikonda stendi. Usafiri kutoka Mbeya na Makete mjini kupitia Ikonda upo kwa mabasi ya kampuni za **Super Rojas, Japanese express, Ilininda na Masihi.** **IZINGATIWE KUWA** *Ukitoka Njombe au Mbeya lazima ushukie stendi ya Ikonda madukani ndipo ufike shuleni (makete girls sec. school) na ukikosa basi panda boda.* (Nauli ya boda isizidi 7,000)

**2.0 MAHITAJI**

Yafuatayo ni maagizo/mahitaji/michango/na vifaa muhimu ambavyo ni lazima ujenavyo siku unapofika kuripoti hapa shuleni.

**2.1 MICHANGO YA SHULE**

(a) michango ya uendeshaji shule Tsh. 65,000/=
(b) Tahadhali Tsh. 5,000/=
(c) Nembo Tsh. 5,000/=
(d) Kitambulisho Tsh. 5,000/= **JUMLA TSH. 80,000/=**

**<u>MUHIMU</u>**

- Michango kwa mwaka mzima ni Tsh. 80,000/= michango yote inatakiwa ilipwe awamu ya kwanza

- FEDHA HIZI ZOTE ZILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE (NMB 60410002450, MAKETE GIRLS SECONDARY SCHOOL)
- Andika jina la mwanafunzi anayelipa, darasa na mchepuo na orodhesha vitu vilivyolipiwa. Hatupokei fedha mkononi. Uje na hiyo risiti (BPS) hapa shuleni.
- MATIBABU YA MTOTO NI JUKUMU LA MZAZI NA SI LA SHULE.

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

**2.2 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**A. SARE ZA SHULE NA MAHITAJI MENGINE.**

i Sketi mbili rangi ya bluu nyeusi (darkblue) kitambaa kizito ziwe ndefu

ii Uje na shati mbili nyeupe za mikono mirefu.

iii Uje na magauni mawili (2) rangi ya udongo, kitambaa kizito, mshono wa solo.

iv. Jacket moja zito jeusi lenye kofia lisilo na maandishi yoyote kwa ajili ya kujikinga na baridi, majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi kabisa

v. Pull neck nyeusi (kabashingo).

vi. Uje na hijabu ya rangi nyeupe. Hii ni kwa waislamu tu.

vii. Uje na truck suit ya bluu nyeusi (darkbluu) zenye ufito mweupe.

viii. Uje na nguo za michezo: raba, bukta na t-sheti zifanane (Nyekundu au nyeupe) kwa ajili ya michezo na mazoezi.

ix. Uje na viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili visivyo na kisigino kirefu.

x. Uje na soksi nyeupe ndefu jozi nne au zaidi.

xi. Sweta mbili za blue nyeusi (dark bluu) (zenye mshono wa V shingoni

xii. T-shirt yenye nembo ya shule. Inapatikana shuleni.

xiii. Uje na taulo za kike za kutosha (Pedi), pea moja ya kanga au kitenge.

xiv. Mahitaji mengine ni godoro nchi 2.5, blanketi moja na mashuka mawili (moja la pink na moja la bluu bahari) tranka kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake, taulo, ndoo 2 zenye mifuniko moja ya kuogea na moja ya usafi wa mazingira, kontena, kijiko, kikombe, dawa ya meno na mswaki, kiwi ya viatu na ndala.

xv. Aje na jembe 1, cherewa 1, na wanafunzi wa kombi ya **HGK** na **HKL** waje na sabuni ya maji lita 5 aina ya **TARMOL** au **DEX**, wanafunzi wa **HGLi** na **HGFa** waje na Hardbloom 1, soft Bloom, Mopa.

**B. MAWASILIANO YA SHULE**

i. Barua S.L.P 36, MAKETE

ii. **SIMU YA SHULE 0799881784** kwa ajili ya mawasiliano yao na wazazi/walezi wa wanapokuwa na matatizo au kuomba fedha za matumizi. Namba hizi hutumika kwa mawasiliano na kutuma fedha. Andika Jina la mwanafunzi unayemtumia, Na kidato chake.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu au laini shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**C. VIFAA VYA KITAALUMA**

i. Daftari counter books 10 kwa ajili ya notes za masomo yake (akiweza aje na fedha atapata hapa shuleni) school bag ni lazima kwa ajili ya kuhifadhia madaftari hayo.

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

ii. Advanced Dictionary kwa wote iii. Wanaochukua Tahasusi yenye Kiswahili waje na kamusi na wanaochukua Tahasusi yenye Geography waje na Atlas.
iv. Rim A4 2 bunda moja 01 kila muhula

**ENGLISH LANGUAGE**

a) James J (2012, Advanced English Language, form six and form five, Oxford university press.
b) Asheri N. (2010) advanced level English Second Edition, Good book publisher, Dar-es-salaam. Advanced literature

**NOVELS**

1. Animal farm – George orwell
2. Chasing the Leopard finding the Lion – Julie Wakeman- Linn
3. The Opportunist Elite – Nyambari C.M. Nyangwine
4. The horizon Unveiled – Fellowes Mwaisela

**PLAYS**

1. An enemy of the people – Henrick Ibsen
2. The bride – Austin Bukenya
3. The government inspector – Nikolai V. Gogol

**POETRY**

1. Summons: poems from Tanzania - Rashid S. Mabala et al.
2. Poets of Africa: Lament of the silent & other poems – Jared Angira.

**VITABU VYA KISWAHILI**

**USHAIRI**

a) Fumbo linalo elea – Nyambari C.M Nyangwine
b) Malenga wa Ziwa Kuu – Wallah Bin Wallah
c) Andamo, Msafiri Safarin – Mohammed Khelef Ghassani.
d) Wosia wa Baba – Ahmed Mchamed Amanzy

**RIWAYA**

a) Dunia uwanja wa fujo – Euphrase Kezilahabi
b) Ua la Faraja – W.E Mkufya
c) Mirathi ya Hatari – C.G. Mung'ong'o
d) Wasifu Wasiti Binti Saad – Shaban Robert

**TAMTHILIYA**

**a)** Mkwava wa Uhehe – M.M. Mulokozi.
**b)** Shujaa Mirambo – Emmanuel Mbogo
**c)** Usaliti Mjini – Francis Imbuga

**FASIHI YA KISWAHILI (Fa)**

**RIWAYA**

a) Vuta Nkuvute – Shafi Adam Shafi

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

b) Asali Chungu – Said Ahmed Mohamed
c) Mwana wa Yungi Hulewa – Mohammed Said Abdulla
d) Vipuli Vya Figo – Emmanuel Mbogo

**TAMTHILIYA**

a) Kaptula la Max – Euphrase Kezilahabi
b) Nyerere na safari ya kanani – Emmanuel Mbogo
c) Morani – Emmanuel Mbogo

**USHAIRI**

a) Dhifa – Euphrase Kezilahabi
b) Utenzi Majumui wa Karne ya 21 – Idd M. Mwimbe
c) Malenga wa Bara – M.M. Mulokozi na K.K. Kahigi
d) Fungate ya Uhuru – Mohamed Seif Khatibu.

**LITERATURE IN INGLISH (Li)**
**NOVEL**

a) Arrow of God – Chinua Achebe
b) A man of the people – Chinua Achebe
c) A grain of Wheat – Ngugi wa Thiong'o
d) Petals of Blood – Ngugu wa Thiong'o
e) No Longer at Ease – Chinua Achebe
f) Joy Comes in the Morning – Hopolang Phororo
g) The Lion of Yola – Severine Ndunguru

**PLAY**

a) Betrayal in the City – Frrancis Imbuga
b) I Will Marry When I Want – Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa mirii
c) Julius Caesar – William Shakespeare
d) Man of Kafira – Francis Imbuga

**POETRY**

a) Poets of Africa 7; Boundless Voices poem from Kenya – Arthur I. Luvai
b) The Bleeding Heart and Other Poems – Shilla Kaaya

**3. SIMU ZA WALEZI WAO (WALIMU)**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

a) Mkuu wa shule - **0766 252 580 / 0679 331 532**
b) Makamu mkuu wa shule - **0674742194**
c) Mhasibu wa shule - **0719546839**
d) Malezi – **0799881784**

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

e) Taaluma – **0657 808 578**

**MAELEKEZO MUHIMU**

a) Baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kutelekeza watoto wao bila kuwapa mahitaji muhimu na fedha za matumizi wakiwa hapa shuleni hivi kuleta usumbufu kwa shule kwa kuwa omba omba wakifikiri shule ina utaratibu wa kuwa na fedha kitu hicho hakipo ni jukumu lako mzazi/mlezi kumpa fedha za mahitaji yake kupitia simu ya shule.

b) Baadhi ya wanafunzi wamekuwa na tabia ya kukataa, kufanya kazi za nje kama usafi wa bweni, kufyeka n.k. shule haitavumilia tabia hiyo. Shule haitakuwa na huruma kwa mwanafunzi wa aina hii. Mwanafunzi lazima afundishwe Elimu ya kujitegemea. Na hii ndio sera ya taifa letu atafanya kazi zote za shule.

c) SIMU, ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu shuleni na kutumia vifaa vya muziki na camera shuleni. Mawasiliano yote ni kwa kupitia shule kwa namba tulizoorodhesha. Ni vizuri ukalielewa hili vizuri na hatutakuwa na huruma katika suala hili.

d) Usifike bwenini bila kuripoti ofisi ya Mkuu wa shule au Makamu mkuu wa shule.

e) Bank paying-slips ziwasilishwe kwa mhasibu wa shule hapa shuleni na si kwingine.
Hakikisha unapewa stakabadhi. Ahadi za kulipa baadaye hazitasikilizwa.

f) Vazi la shule lazima livaliwe wakati wote wa masomo na kwenye shughuli rasmi. Mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi kabisa uwapo shuleni.

g) Maagizo ya fedha (karo na michango yote) na mahitaji yote muhimu vyote vitakaguliwa mara tu mwanafunzi atakapofika kujiunga na shule hii, visipokamilika mwanafunzi atarudishwa nyumbani kuvifuata.

h) Ni marufuku kuja na kofia, pete na mapambo mengine au mitindo isiyofaa ya kunyoa nywele.

i) Hairuhusiwi kufuga nywele, muda wote nywele ziwe fupi.

j) Ikiwezekana mfungulie Akaunti NMB au atafungua akiwa hapa shuleni kwa kushirikiana na Benki ya NMB au CRDB Makete.

k) Hatutaruhusu mwanafunzi kubaki wakati wa likizo hakikisha mzazi unatuma nauli mapema, sababu ni kwamba chakula cha kuwalisha wanafunzi hakipo wakati wa likizo.

l) AFYA Unatakiwa kupima afya yako kabla ya kuripoti shuleni, fomu maalum imeambatanishwa kwa ajili hiyo na utatakiwa kukabidhi fomu hiyo iliyokamilika mara tu ufikapo shuleni.
Kama una matatizo ya muda mrefu ya kiafya toa taarifa ufikapo shuleni. Vyeti ni lazima uje navyo kama una matatizo sugu. Shule haina uwezo wa kutoa chakula maalum cha wagonjwa wakudumu. Shule haitavulimilia mwanafunzi anayejisingizia ugonjwa kwa sababu zake binafsi. Fomu ya daktari itatumika katika maamuzi yote.
Mwanafunzi aje na Bima ya Afya kama anayo, ambaye hana anashauriwa kujiunga kwenye Bima za kikaya CHF kwa mwaka.

**5. UHURU WA KUABUDU**

Utaruhusiwa kuabudu kwa kadri ya dini kwa kufuata sheria, ratiba na taratibu za shule na za nchi ingawa tabia ya kubughudhi wengine haitavumiliwa. Ukitaka

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

kubadili dini ukiwa shuleni utatakiwa kuleta uthibitisho wa barua kutoka kwa mzazi wako. Shule yetu ni ya mchanganyiko wa Dini, pia kumbuka serikali haina dini hivyo shule haitakubali kuleta taratibu Fulani ili kubugudhi wengine.

**6. KUBADILI JINA**

Hautaruhusiwa kubadili jina lako litatakiwa kutumika kama lilivyotumika wakati wa mtihani wa kidato cha nne (4) au kama lilivyo kwenye Sel-form yako. Ili kupunguza usumbufu wa usajili katika kipengere hiki mwanafunzi anaporipoti anatakiwa kuja na nakala halisi na si copy ya cheti. Result Slips (origin).

**7. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

a) Wizi
b) Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 (utoro) bila taarifa.
c) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzie, walezi na wakubwa
d) Kugoma na kuhamasisha mgomo
e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi au kumpiga mwalimu
f) Uasherati, kujihusisha na mapenzi hapa shuleni au kutoa mimba
g) Kuoa au kuolewa
h) Kutembelea majumba ya starehe guest house, bar
i) Ulevi/madawa ya kulevya (kutumia) au kukutwa nayo.
j) Kudharau bendera ya Taifa.
k) Kumiliki simu ya mkononi shuleni.
l) Kuharibu mali za shule kwa makusudi au kuuza mali za shule.
m) Kugoma kufanya kazi halali za shule ambazo ni kwa manufaa yao na ustawi wao hapa shuleni.
n) Kuondoka shule kabla ya muda halali wa serikali na kutohudhuria Baraza la kufungia shule.
o) Kujihusisha na mapenzi ya jinsi moja.



**SAYUNI EMBASY SANGA**
**MKUU WA SHULE**

Nakala Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
S.L.P 06,
**MAKETE,**

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI MAKETE WASICHANA**

**FOMU YA MAPATANO/KUKUBALI NAFASI YA MASOMO NA KUSOMA KATIKA SHULE HII KIDATO CHA __________ MWAKA__________**

NB: Kabla ya kusaini soma kwa makini maagizo yote kama hutaridhika basi usifike kabisa. Tafuta shule yoyote Tanzania. Shule haitasikiliza vizingizio vya aina yoyote. pia kama afya yako si nzuri fanya utaratibu na mzazi wako kupata shule nyingine ukiwa huko huko shule haitataka usumbufu wowote. Au KAMA unataka masomo ambayo shule hii hayapo wasiliana na wizara ili ubadilishwe huko huko.

**JINA LA MWANAFUNZI ____________________________________________**
**ANWANI:____________________________________________________________**
**MIMI_______________________________________________________________**

Nimekubali/sikubali kujiunga na Jamuiya ya shule ya sekondari MAKETE WASICHANA. Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa, Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Kinyume chake hatua kali zitachukuliwa dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Naahidi kusoma kwa bidii sana masomo yangu na kufaulu mitihani itakayotolewa na shule, Mkoa na

Taifa.

Sahihi ya mwanafunzi _________________________________

Tarehe_________________________ B. Mzazi/mlezi

Mimi nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa mtoto wangu nimekubali /sikubali mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia, Naahidi pia kumlipia karo ya shule/fedha za matibabu/na michango mingine mbalimbali iliyoagizwa na shule kwa wakati mwafaka kinyume chake nichukuliwe hatua za kisheria.

Sahihi ya mzazi /mlezi ____________________ Tarehe ___________________ NB:

Fomu hii itawekwa kwenye faili lake.

Andika namba ya simu ya mzazi _________________ kwa ajili ya mawasiliano na shule.

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

**SEHEMU YA MGANGA**

**THE PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MAKETE GIRLS SECONDARY SCHOOL**
**(REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)**

This form must be completed by a Government Medical Officer.
Name of student ……………………………………………………………………………
Age ………………………………………………………… Sex ……………………………

The above named student has been examined in respect of:

a) PREGNANT TEST: ……………………………………………………………………
b) STOOL: ……………………………………………………………………………………
c) URINE: ………………………………………………………………………
d) CHEST: ……………………………………………………………………………………
e) BLOOD: …………………………………………………………………………………
f) EYES: ……………………………………………………………………………………
g) EARS: ……………………………………………………………………………………
h) HEAMAGLOBIN: ………………………………………………………………………
i) P. V. BLEEDING
j) ASTHMA: …………………………………………………………………………………
k) SKIN DESTASL: ………………………………………………………………………
l) LEPROSY: ………………………………………………………………………………
m) ETHEPSY: ………………………………………………………………………………
n) ANY DEFORMITY
o) T.B: ……………………………………………………………………………………
p) NEUROSIS: ………………………………………………………………………………
q) VENEREAL DISEASE: ………………………………………………………………
r) OTHER FINDINGS: …………………………………………………………………

I am satisfied that the above student is fit/not fit for pursuing secondary studies at MAKETE GIRLS SECONDARY SCHOOL.

DATE: …………. Name and signature (medical officer): ………………………………………

Designation: ………………………………………… Official stamp ………………………………

MAKETE GIRLS SEC. SCHOOL

**SAMPLE YA SARE YA SHULE**





MAKETE GIRLS S